JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

SHULE YA SEKONDARI MONDO,
S.L.P 88,
CHEMBA,
JUNE 2022.

Mkuu wa Shule +255759957947
M/mkuu wa Shule: +255786226927
Mtaaluma: +255623684893
Barua Pepe: magrethrodgers586@gmail.com
kalistisseverini@gmail.com

KUMB. Na: MDSS/ DO/ ADM/ F. V/ 2022

JINA LA MWANAFUNZI…….
S.L.P…….
……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MONDO WILAYA YA CHEMBA MKOA WA DODOMA MWAKA 2022

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Tano, kwa** Tahasusi ya…….. **.** katika shule **ya Sekondari ya Mondo** mwaka **2022.**
Shule ipo katika Tarafa ya **Mondo**, Wilaya ya **Chemba** na Mkoa wa **Dodoma**.
Unaweza kufika shuleni kwa kupanda basi stendi ya Chang'ombe au stendi ya Machame, iliyopo Dodoma mjini kila siku saa 4:30 asubuhi na utashuka stendi ya Mondo.Umbali ni km137 sawa na nauli ya Tsh.8000/= . Aidha, unaweza kufika Mondo Sekondari kwa kupanda Basi linalopita Mondo kutoka Stendi ya Mabasi Kondoa Mjini. Umbali ni km 20 sawa na nauli ya Tsh.2000/= na utashuka standi ya Mondo. Kutoka hapo utatembea kwa mguu mwendo mfupi wa mita 400 kufika shuleni.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe …… unatakiwa kuripoti shuleni

Edit with WPS Office

kuanzia tarehe ..... na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe ……

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare/ mahitaji yafuatayo:-**

(i) Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu na yasiyo bana mwili. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na **JUBA** mbili (2) nyeupe ndefu zenye kufunika kifua mpaka kwenye vifundo vya mikono na zisizo na marembo yoyote.

(ii) Sketi mbili (2) za rangi ya darkblue (blue nyeusi) mshono wa RINDA BOX kubwa mbele na nyuma na mawili kushoto na kulia mawili na tai mbili zenye rangi ya sketi (dark blue), urefu wa sketi ufike kwenye vifundo vya miguu, kitambaa **kizito cha suti.**

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi. **Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote.**

(iv) Jozi mbili (2) za soksi nyeupe zisizo na mistari yoyote.

(v) Nguo za kushindia gauni la drafti ndogo ya dark blue ambalo litapatikana shuleni kwa shilingi elfu ishirini na tano tu (25000/=),kwa wanafunzi wa kiislamu juba ya blue bahari, T-shirt ya blue yenye kola itapatikana shule kwa bei ya shilingi elfu kumi na tano tu(Tsh 15000/=).

(vi) Sweta moja (1)ya rangi ya dark blue inayofanana na sketi za shule.

(vii) Shuka mbili (2) rangi ya blue bahari (light blue) na blanketi moja.

(viii) Godoro la ukubwa wa futi 2.5x6 ambalo litapatikana shuleni kwa shilingi elfu hamsini (50000/=)

(ix) Taulo, Vitenge au Kanga doti moja atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

(x) Tracksuit rangi ya blue bahari (light blue) Jozi moja (atavaa wakati wa maandalio ya usiku na michezo

(xi) Tranka (sanduku la chuma)1 kwa ajili ya usalama wa vitu vyake na kufuli imara kwa ajili ya kufungia tranka.

(xii) Chandarua rangi ya light blue

(xiii) Raba za michezo rangi nyeupe

Edit with WPS Office

2.2 Mahitaji mengine ya mwanafunzi

(i) Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe na bakuli)

(ii) Picha 4 passport size (kwa ajili ya kurahisisha utengenezaji wa kitambulisho zitapigwa shule)

(iii) Madaftari 11 (counter Book) quire 3 au 4, kalamu za risasi na za wino na mkebe wa
vifaa vya Hisabati (Mathematical set).

(iv) Calculator kwa wanaosoma masomo ya Sayansi na Hesabu (scientific calculator)

(v) Dissection kit kwa wanafunzi wa mchepuo wa (PCB na CBG), laboratory coat, eye protector-goggles, na laboratory masks kwa wanafunzi wote wa michepuo ya sayansi.

N.B: Vifaa vilivyotajwa hapo juu (2.2, i-iv) vitapatikana shuleni kwa gharama stahiki endapo mwanafunzi atakuwa amevikosa.

Njoo na vifaa vifuatavyo:-

1. Jembe na mpini (01)
2. Fyekeo (01)
3. Ufagio wa ndani mrefu (01)
4. Squeezer (mopper) (01)
5. Ndoo 2 (lita 20 moja na lita 10 moja)
6. **Result slip ya matokeo ya kidato cha nne. (original copy)**
7. **Nakala ya cheti cha kuzaliwa.**
8. Ream mbili (2) kwa mwaka

Vifaa tajwa hapo juu(1,2,3,4,5 na 8) vinapatikana shuleni kama mwanafunzi ataona usumbufu wa kubeba.

KUMBUKA: * Simu haziruhusiwi shuleni.

*** Mwanafunzi analazimika kuvaa vazi la shule wakati wote awapo shuleni, hivyo asije na nguo za nyumbani .**

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Tekinolojia yenye dhamana ya usimamizi wa Elimu. Aidha Ofisi ya Rais– TAMISEMI ina jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii

Edit with WPS Office

kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;

(i) Kutunza mali za shule.

MUHIMU:

1. Mwanafunzi ataruhusiwa kuja/kurudi nyumbani Kwa ajili ya msiba wa mama, baba,mlezi, kaka au dada tu na siyo mtu mwingine. Taarifa za misiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi. Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.
2. Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula katika Bwalo.
3. Wageni wanao tambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja kwa kila muhula yaani mara 2 kwa mwaka.
4. Likizo zote mwanafunzi atalazimika kwenda nyumbani.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi.
2. Uasherati, ushoga na usagaji.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa.
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. **Kuwa na simu ya mkononi shuleni.**

Edit with WPS Office

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI.

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Medical ExaminationForm) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kwa kikamilifu.

A: MICHANGO

1. Ada/ Karo ya Shule

NA	Fedha kwa ajili ya	Kiasi kinachotakiwa	Jina na Namba ya Akaunti
1.	Ada/ Karo ya Shule	Kwa mwaka ni Sh. 70,000/= Au Sh. 35,000/= Kwa Muhula	KDC MONDO SECONDARY SCHOOL. NMB KONDOA Branch A/C Na: 50201200071

2. Michango Mingine

Na.	Fedha kwa ajili ya:-	Kiasi kinachohitajika	Jina na Namba ya Akaunti
1.	Tahadhari	Sh. 10,000/= (Hairudishwi)	MONDO SECONDARY SCHOOLHARP A/CNMB KONDOA Branch A/C Na. 50202300326.
2.	Kitambulisho na picha nne	Sh.8000/= (Mara moja)	
4.	Wapishi na Walinzi	Sh.20,000/=(Kwa mwaka)	
5.	Huduma ya kwanza(afya)	Sh. 20,000/= (kwa Mwaka)	
6.	Taaluma	Sh.15,000/=(kwa mwaka)	
7.	Mahafali	Sh.	
8.	Vifaa na kemikali za maabara	Tsh. 20,000/= (kwa mwaka)	
9.	Maji	Tsh. 20,000/=(kwa mwaka)	
10.	Michezo (UMISETA)	Tsh. 5,000/= kwa mwaka	
	JUMLA	Sh.118,000 /=	

Edit with WPS Office

Edit with WPS Office

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENTS' OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MONDO SECONDARY SCHOOL,
MEDICAL EXAMINATIONFORM

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name……

Age/Years……Sex……

Blood found (red and White)…….

Stool examination:…….

Urinalysis:……..

Venereal Diseases test:……..

T.B. test:……

Eye Test:……

Ears:……

Chest:…….

Spleen:……

Abdomen:……..

Urine for Pregnant:……

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

……..

……..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:……..

Designation:……..

Station:……Date:……

Official Stamp: ……

Edit with WPS Office

FORM NO. 2
SHULE YA SEKONDARI YA MONDO
TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI……..
2. KABILA……...
3. TAREHE YA KUZALIWA…….MWEZI……MWAKA…….
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA…….
   MKOA WA……..
5. DINI……DHEHEBU……....
6. JINA LA MZAZI/MLEZI……
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI……(KIJIJI)
   ……. (TARAFA)
   …… (WILAYA)
   ……. (MKOA)
   Na. ya simu…….
8. KAZI YA BABA/MLEZI……
9. KAZI YA MAMA……...
10. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
    ……
    ……
    ……
11. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za Simu.

(a) Ndugu(1)……Uhusiano…… Namba za simu……..
……..
(b) Ndugu(2)…… Uhusiano……Namba za simu…….
……..
(c) Ndugu(3)…… … Uhusiano……Namba za simu……..
……

SAINI YA MWANAFUNZI **SAINI YA MZAZI/MLEZI**

TAREHE:…… TAREHE:……

Edit with WPS Office

FORM NO.3
SHULE YA SEKONDARI YA MONDO

MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi……. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Nahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi…….

Tarehe……

Shahidi

Jina kamili……..

Saini…….

Tarehe……..

Edit with WPS Office

SHULE YA SEKONDARI YA MONDO

FORM NO. 4

A: AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi…… (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……..Kidato cha……. Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubalianana yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya Mzazi/Mlezi…….

Anuani kamili…….

Simu:……

Tarehe:…….

Edit with WPS Office